


**Waambie familia yako kuhusu  
habari hii**

**Karibu!**

**Sasa kwa kuwa nipo Marekani, nini kitatokea kuhusiana na kesi yangu ya uhamiaji?**



**1. Nenda kwenye za ukaguzi wako wa ICE**

Ukaguzi huu ni kwa ajili ya ICE kufuatilia eneo lako unapokuwa Marekani wakati kesi yako inasubiri kisikilizwa mahakamani. Kutoenda kwenye ukaguzi wako wa ICE kunaweza kusababisha ICE ikurudishe kwenye kituo cha kizuizini.

**2. Nenda kwenye za miadi (kusikilizwa kesi) yako ya Mahakama ya Uhamiaji**

Miadi hii (au usikilizaji wa kesi) ni kwa ajili ya kuamua ikiwa utaweza kubaki Marekani kihalali, au ikiwa italazimika urudi nchini kwako. Ikiwa hautaenda kwenye miadi yako, kuna uwezekano mkubwa kwamba jaji atakuamuru urudishwe nchini mwako kwa sababu hukuonekana kwenye kesi yako.

**Je, ni lini natakiwa kwenda katika mahakama ya Uhamiaji?**

Ndani ya wiki mbili unapaswa kupokea barua na maelezo juu ya kusikiliza kesi yako kwa mara ya kwanza katika mahakama ya uhamiaji. (Barua hii inapaswa kuja katika anwani ya mdhamini wako ambayo inaonekana katika hati uliyopewa mpakani.) Wakati uo huo, wapigie simu mahakama ya uhamiaji kupitia 11-800-898-7180 angalau mara moja kwa wiki - unaweza kujua tarehe ya miadi yako ya kwanza ya mahakamani kwa kupiga simu kabla ya kupokea barua ikiwa na taarifa hiyo.

- Piga **1-800-898-7180**. Bonyeza **1** kwa maagizo katika Kiingereza (au **2** kwa maagizo katika Kihispania).
- Baada ya maagizo kukamilika, ingiza nambari yako ya A
  - Kutafuta habari, itabidi utafute **na nambari A yako**, si kwa jina lako.
  - Nambari A yako inaonekana kwenye hati ulizopewa mpakani.
    - Nambari A yako: \_\_\_\_\_
    - Nambari A ya mwenzi wako (ikiwa yuko hapa na wewe):  
\_\_\_\_\_

## Waambie familia yako kuhusu habari hii

- Nambari A za mtoto/ watoto wako: \_\_\_\_\_,  
\_\_\_\_\_, \_\_\_\_\_
- Inawezekana kwamba shauri lako la mahakama litakuwa katika tarehe moja na mwenzi wako na / au mtoto/ watoto wako. Lakini ni muhimu kupiga 11-800-898-7180 mara moja kwa wiki kwa kila mwanafamilia wako.

### Je, itakuwaje ikiwa sina mwanasheria wa kwenda naye mahakamani kusikiliza shauri langu la kwanza?

Usiogope! Kesi yako haitaamuliwa katika shauri la kwanza. Unaweza kumwomba jaji akupe muda zaidi ili umtafute wakili. Jaji atakupangia shauri la pili kwa tarehe za baadaye.

### Nani anaweza kunisaidia kesi yangu?

Hapa chini kuna orodha ya mashirika ambayo yanazisaidia jamii za wahamiaji. Mara baada ya kuwasili kwenye kituo chako cha mwisho, unapaswa kuwasiliana na mashirika haya. Unachopaswa kufanya ni kusema kitu kama:

*"Habari, jina langu ni \_\_\_\_\_. Nilikuwa mpakani na mtoto / watoto wangu kwa siku \_\_\_\_\_, na ninasubiri taarifa kuhusu shauri langu kusikilizwa mahakamani. Nina maswali na ninahitaji kuongea na mtu kuhusu kesi yangu ya Uhamiaji. "*

Kwa sasa kuna mahitaji makubwa ya huduma za kisheria kwa hivyo kuna uwezekano mkubwa kwamba itabidi usubiri wiki kadhaa (au zaidi) ili kupata miadi na wakili au msaidizi wa kisheria. Ni muhimu kupiga simu kwenye mashirika kadhaa. Tafadhali kuwa na subira, na ikiwa umepewa nafasi kwenye orodha ya kusubiri, ichukue. Na unapokuwa na miadi yako na wakili au msaidizi wa kisheria, ni muhimu sana kujibu maswali yao yote kwa kuwaambia kila kitu na kuwapatia maelezo kuhusu hali yako, hata ikiwa ni vigumu kuongea - usiogope, wapo kwa ajili ya kukusaidia.

Kumbuka kwamba hapa Marekani **notario SI mwanasheria**. Kuna watu ambao wanajionesha kana kwamba ni wanasheria lakini kwa kweli sio. Pia kuna wanasheria ambao ni wanasheria kweli lakini ambao si weledi katika sheria za uhamiaji. Kwa hivyo ni muhimu sana kuwasiliana na mashirika kama haya yaliyoorodheshwa hapa chini ambayo yana weledi katika kusaidia wahamiaji - mashirika haya yanaaminika na ni bora zaidi, na hayatozi ada kwa huduma zao.